# DARUBINI

# Kuendeleza Uwajibikaji na Usimamizi Sekta ya Mafuta na Gesi: Mradi wa Gesi Asilia Tanzania (LNG)




Toleo la 5
Agosti 2024

Imedhaminiwa na: Belgium partner in development

Imechapishwa na:
HakiRasilimali, International Peace Information Services (IPIS),
Business Human Rights Tanzania (BHRT) & Avocats Sans Frontières (ASF)

# Kuendeleza Uwajibikaji na Usimamizi Sekta ya Mafuta na Gesi: Mradi wa Gesi Asilia Tanzania (LNG)

## Utangulizi

Tanzania iko karibu kufikia makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa gesi asilia kwa kushirikiana na makampuni ya kimataifa. Hata hivyo, dunia inakabiliwa na changamoto kubwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, uharibifu wa mazingira, na hitaji la kuhamia kwenye vyanzo vya nishati safi na endelevu.

Mazingira ya nishati duniani yanapitia mabadiliko makubwa (Hussein, 2023). Mhamo wa nishati huhusisha kuepukana na matumizi ya vyanzo vya nishati vinavyo zalisha hewa ya Ukaa mfano, makaa ya mawe na mafuta kwenda katika vyanzo vya nishati safi kama vile nishati ya upepo, jua na umeme wa maji. Swala hili la mhamo wa nishati kwa nafasi kubwa hutoa taswira ya kufikirisha nchini Tanzania kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha gesi asilia ambayo hutambuliwa kama nishati mpito kutokana na uzalishaji wake mdogo wa hewa ya Kaboni (The Citizen, 2023). Pamoja na hayo yote, dunia bado inapambana kwa nguvu kupunguza uzalishaji wa gesi chafu ili kupunguza athari zake. Swala la uwajibikaji limekuwa na umuhimu mkubwa, hasa katika uendelezaji na matumizi ya gesi asilia nchini Tanzania, ili kuendana na jitihada za utunzaji wa mazingira kwa ajili ya mustakabali wa nishati endelevu (Nakanagwi , 2021).

Mradi wa gesi asilia uliopo Likong'o unatokana na kugunduliwa kwa kiasi cha futi za ujazo trilioni 57 za gesi asilia ndani ya Bahari ya Hindi. Mradi huu umelenga hasa kusafirisha gesi hiyo nje ya nchi (Tanzania Invest, 2023). Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linashirikiana na makampuni ya kimataifa, ikiwemo Equinor, ExxonMobil, na Shell, katika uwekezaji wa mradi huu wenye thamani ya jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 42 (Tanzania Invest, 2023).

Kwa hivyo, ripoti hii inaangazia mradi wa gesi asilia katika nyanja mbalimbali ili kubaini uhalisia wa uhusiano wake na masuala ya kimazingira, ushirikishwaji wa jamii, uhusiano wa kiuchumi na kisera uliopo, pamoja na maendeleo endelevu ya kijamii. Mwishowe, ripoti inatoa mapendekezo juu ya nishati mpito unaozingatia haki katika utekelezaji wake.

## Ulinganifu wa Gesi Asilia (LNG) na Nishati Mbadala (RES) kwa Mustakabali Endelevu

Tanzania inategemea kwa kiasi kikubwa nishati ya mafuta. Hivyo, kubadilisha vyanzo vya nishati na kuelekea kwenye nishati mbadala ni jambo la lazima na linapaswa kupewa kipaumbele. Hii itasaidia kuhakikisha uwepo wa rasilimali za nishati endelevu kwa siku zijazo.

Licha ya kusafirisha nishati mbalimbali kama vile makaa ya mawe kwenye masoko ya kimataifa, taifa limeonesha hali ya utambuzi wa umuhimu wa kupunguza vyanzo hivi vya nishati chafu.

Mathalani, uwepo wa Mpango Mkuu wa Mfumo wa Kitaifa wa Nishati (PSMP) unaelezea malengo kabambe ya kuleta nishati mseto ifikapo mwaka 2044 (Wizara ya Nishati, 2020). Vilevile, mpango huu unaangazia jukumu muhimu la uwekezaji wa kigeni katika mifumo ya nishati mbadala.

Hifadhi ya gesi asilia nchini inawakilisha chanzo kikubwa cha gesi asilia inayotoa manufaa mbalimbali kwa taifa. Inachangia kwa kiasi kikubwa katika nishati mseto, kupunguza utegemezi wa nishati chafu, na kuchochea mhamo wa nishati kwa kuhakikisha hali ya uwajibikaji (Stanbic, 2020). Hadi kufikia mwaka 2023, uwezo wa gridi ya taifa ulikuwa MW 1,899.05. Katika jumla hiyo, MW 1,193.82 (63%) huzalishwa kwa kutumia gesi asilia, MW 601.60 (32%) zinatokana na nishati ya maji, MW 83.93 (4%) huzalishwa kwa kutumia mafuta, na MW 10.5 (chini ya 1%) zinatokana na bayomasi, ikijumuisha nishati inayotokana na mimea, wanyama, na taka za kilimo (Tanzania Invest, 2024).

Uchambuzi wa kina ulifanyika ili kutoa hali ya ulinganifu kati ya nishati ya gesi asilia na vyanzo vya nishati mbadala, ukichambua ubora, udhaifu, fursa, na hatari zinazohusiana na vyanzo hivi vya nishati. Ulinganifu huu unaonesha kuwa gesi asilia, ingawa inanufaika kutokana na jiografia nzuri na ufanyaji kazi wake kama nishati mpito, inakabiliwa na changamoto kubwa kutokana na uzalishaji wa methane, ambayo inachangia mabadiliko ya tabia nchi (Al -Hai dus, 2022).

Tofauti na hivyo, nishati mbadala ni safi na endelevu, ingawa inakabiliwa na changamoto za vipindi na gharama kubwa za usakinishaji. Fursa za gesi asilia zinajumuisha kuvutia uwekezaji wa kigeni na kuimarisha uhusiano wa viwanda vya ndani, wakati nishati mbadala ina gharama ndogo za uendeshaji na faida kubwa za uhifadhi wa mazingira. Vyanzo vyote viwili vya nishati vinakabiliwa na hatari tofauti, kama vile changamoto za udhibiti na usimamizi wa gesi asilia na masuala ya uunganishaji wa miundombinu kwa nishati mbadala (Al -Hai dus, 2022).

Aidha, tatizo la nishati nchini Tanzania linahitaji mkakati madhubuti wa kitaifa wa kuhamia kutoka kwenye nishati mpito kuelekea vyanzo vya nishati safi. Japokuwa nishati ya gesi asilia (LNG) inatoa suluhu kwa kuwa na uzalishaji mdogo wa kaboni ikilinganishwa na makaa ya mawe, bado si chaguo sahihi sana kwa kuzingatia hali ya uendelevu kwa muda mrefu (Rayna Skiver, 2022). Mkakati unapaswa kulenga zaidi jitihada za kuhamia kwenye mifumo ya nishati mbadala ili kuongeza faida za matumizi ya nishati safi na endelevu, licha ya changamoto za vipindi na gharama kubwa za awali za usanikishaji. Katika muktadha huu, matumizi ya gesi asilia kama hatua za kuelekea kwenye uwekezaji wa nishati mbadala yanaweza kusaidia. Bila shaka, Tanzania inaweza kujihakikishia mustakabali wa nishati unaoaminika, ulio rafiki kwa mazingira, na wa gharama nafuu kwa kuzingatia hatua hizi.

## Uwepo wa Mradi wa Gesi Asilia: Je, ni Changamoto ya Kimaamuzi?

Ugunduzi wa nishati ya gesi asilia ulianza mwaka 2010, na mradi huo umeendelea kwa awamu kadhaa tangu wakati huo.

Kuanzia 2010 hadi 2015, Awamu ya I ilihusisha ugunduzi wa hifadhi kubwa ya gesi asilia na kuweka mazingira ya maendeleo ya baadae. Katika awamu ya pili , kuanzia 2016 hadi 2020, hatua za awali za utekelezaji wa mradi zilichukuliwa, ikiwa ni pamoja na kutangaza mipango ya ujenzi wa mradi na kuanza kwa michakato ya fidia. Hata hivyo, awamu ya Tatu , kuanzia 2021 hadi 2025, vimeonekana vikwazo kadhaa kama vile kuchelewa kwa makubaliano ya kimikataba na tahadhari kuhusu ucheleweshaji wa mradi huo (The EastAfrican, 2024).

Utekelezaji wa mradi wa LNG wa Tanzania unakabiliwa na vikwazo vikubwa vya kimaamuzi. Licha ya maendeleo makubwa kutoka 2010 hadi 2020, simulizi zilizopo zinaonesha uamuzi wa mwisho wa uwekezaji wa mradi unategemewa kufanyika mwaka 2025 (Stanbic, 2022). Hata hivyo, mazingira yaliyopo haya akisi simulizi hizo kwa sababu serikali bado ipo katika mchakato wa mazungumzo kuhusu makubaliano yatakayo ingiwa, na inaonekana kuna mikataba ya kuingiwa (Host Government Agreement-HGA na Cost Production Sharing Agreement- PSA) kabla ya kufikiwa kwa mkataba wa mwisho wa uwekezaji (Final Investment Decision- FID). Vilevile, licha yakuwa makubaliano ya awali (Host Government Agreement) yaliingiwa, bado kuna mchakato wa maboresho yanayokusudiwa kuhakikisha kuwa Serikali na Wawekezaji wananufaika ipasavyo kutokana na makubaliano hayo (Offshore Engineer, 2024).

**"Mradi wa LNG bado haujawa sehemu ya maisha yetu licha ya muongo mmoja wa ahadi ambazo hazijatekelezwa. Katika kuelekea uwekezaji huu wa kigeni, hatujaona faida yoyote inayotokana na uwekezaji huu, isipokuwa fidia iliyoondoa paa zetu za nyasi na badala yake tukaweka mabati."**




*Mazungumzo na Wabunge wa Tanzania*

## Mapendekezo: Ushughulikiaji wa Changamoto za Mradi wa Gesi Asilia (LNG) Kwa Ajili ya Kuendeleza na Kukuza Uwajibikaji na Usimamizi Sekta ya Mafuta na Gesi.

### Kwa Serikali

- Tanzania inapaswa kuweka kipaumbele katika kuhamasisha matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala. Ingawa nchi inategemea nishati ya mafuta, hasa kwa masoko ya nje, kupunguza utegemezi huu ni muhimu kwa mustakabali wa nishati. Uwekezaji katika mifumo ya nishati mbadala kama vile nishati ya jua, upepo, na bayomasi utaweza kubadilisha hali ya nishati mseto na kutoa suluhisho la muda mrefu kwa nishati endelevu.
- Kuharakisha ukamilishaji wa Mkataba wa Serikali Mwenyeji (Host Government Agreement) na Mkataba wa Ugawanaji wa Gharama za Uzalishaji (Cost Production Sharing Agreement) kwa mradi wa gesi asilia. Mikataba hii ni muhimu kwa kuanzisha uzalishaji wa gesi asilia na kuweka mfumo wa udhibiti na usimamizi wa kifedha kwa mauzo ya nje. Ni muhimu kuhakikisha kuwa masharti ya mikataba hii ni ya haki na yanayolenga kutoa manufaa kwa pande zote husika. Hii itavutia uwekezaji zaidi na kuongeza ufanisi wa miradi, na kwa maslahi mapana, kusaidia Tanzania kufikia malengo yake ya mpito wa nishati.
- Kuendesha programu za utoaji elimu zitakazofahamisha jamii kuhusu umuhimu wa mpito wa nishati kuelekea matumizi ya vyanzo vya nishati safi na endelevu. Programu hizi zitasaidia kuongeza ufahamu na kuhamasisha jamii kushiriki katika juhudi za kupunguza utegemezi wa nishati chafu na kuchangia kwenye maendeleo endelevu.

### Kwa Makampuni

- Kushirikiana na serikali katika kutekeleza mikakati ya uhifadhi wa mazingira na kusimamia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ujenzi na uendeshaji wa mradi wa gesi asilia.
- Kutoa mafunzo na nafasi za kazi kwa jamii itakayoguswa na mradi kwa lengo la kuhakikisha jamii ina faidika na mradi ipasavyo.

### Kwa Jamii

- Jamii zinapaswa kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kufanya maamuzi na programu za elimu ili kukuza uelewa wao kwenye masuala ya nishati mpito ikiwemo miradi ya gesi asilia.
- Kushiriki kwa kiasi kikubwa katika programu za kujengeana uwezo na mafunzo yanayotolewa ili kuinua ujuzi wao na kuwafanya waweze kushiriki katika ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Muktadha wa kijamii na kisiasa nchini Tanzania umekuwa ukitoa taswira halisi ya hali ya mradi ambao kwa kiasi kikubwa kuanzishwa kwake ni sababu ya kukua kiuchumi na kuimarisha ustawi wa jamii.

Mazungumzo ya muda mrefu na kuchelewa kwa uwekezaji kumechochea hisia tofauti za hofu kuhusu ujio wa mradi. Watu wanahisi kwamba serikali haijatoa kipaumbele cha kutosha kwa mradi huo, na kuna hisia kwamba jamii inayozunguka mradi inaonekana kusahaulika.

Katika mkoa wa Lindi, matarajio na hali ya wasiwasi vimeenea kwa jamii ya Likong'o inayozunguka mradi wa LNG. Hali hii imekuwa ya kufikirisha sana kwa wakazi ambao wamehamishwa kwenda katika makazi mapya ili kupisha maendeleo ya mradi. Jamii ya Likong'o inajumuisha hasa wavuvi, wakulima wadogo wanaolima kwa ajili ya chakula, na wafanya biashara ndogo ndogo. Uhalisia wa jamii hii ni kwamba wanatatizika kuhusu ujio wa mradi na wanajiuliza kama mradi huu utatekelezwa kweli. Ingawa serikali na wawekezaji wa kigeni wamefanikiwa kutoa fidia kwa wale walioguswa, bado kuna hali ya wazi kabisa ya kutoridhika miongoni mwa wanajamii hao.

Mwanajamii mmoja alionesha kusikitishwa na ukimya wa Rais katika ziara yake alipotembelea mkoani Lindi, alisema

**"Mradi wa LNG umeahidiwa kwetu, lakini Rais alikuja hapa katika maandamano ya siku ya UKIMWI katika viwanja vya Ilulu. Cha kushangaza ni kwamba katika ziara yake, mkuu wa nchi (Rais) hakugusia chochote kuhusu mradi wa LNG, na sisi bado tunasubiri."**

Mwanajamii mmoja alieleza kwa hisia kwamba mabadiliko pekee ambayo yanaweza kujivunia ni kubadilisha dari la nyumba kwa bati, tofauti na zamani ambapo nyasi zilitumika kufunika nyumba. Alisema kwamba hayo ndiyo mabadiliko yaliyojitokeza, tofauti na mabadiliko ya kiuchumi yaliyoahidiwa, "Mradi wa LNG bado haujawa sehemu ya maisha yetu licha ya muongo mmoja wa ahadi ambazo hazijatekelezwa. Katika kuelekea uwekezaji huu wa kigeni, hatujaona faida yoyote inayotokana na uwekezaji huu, isipokuwa fidia iliyoondoa paa zetu za nyasi na badala yake tukaweka mabati."

Athari zinazotokana na utekelezaji wa mradi wa gesi asilia (LNG) zimeanza kujitokeza katika sekta ya kilimo na uvuvi. Kwa wakulima, changamoto kubwa imejitokeza kutokana na kuhamishwa na kupoteza ardhi na mashamba yenye rutuba. Hali ni sawa kwa wavuvi ambao wamezuiliwa kuvua katika maeneo yao ya awali kabla ya kuanza kwa mradi.

Changamoto ya kubadili mazao kutoka kilimo cha minazi kwenda kwa mazao kama ufuta na mahindi kumezidisha ugumu wa maisha. Mfano, mtu mwenye umri mkubwa anakumbwa na hofu kuhusu faida ya mazao kama mnazi, ambayo kwa kawaida huchukua muda mrefu kabla ya kutoa matunda.

Katika jitihada za kufanya uchechemuzi katika muktadha wa kisera, kiutawala, na kimaamuzi kuhusu mradi huu wa gesi asilia, wabunge walihusishwa. Wao walieleza kero zao kuhusu maendeleo ya mradi. Kwa mfano, mbunge mmoja alisema:

**"Tumeibua hoja kuhusu wasiwasi uliopo juu ya utekelezaji wa mradi wa gesi asilia, hoja zinazoigusa serikali kuhusu uamuzi wa uwekezaji wa mradi, wa LNG huko Lindi. Na tutaendelea mbele zaidi kuiomba TPDC na Wizara ya Nishati kueleza kwa kina kuhusu swala la ucheleweshaji huo ili tuweze kutambua kinachoendelea nyuma ya pazia."**

Asasi za Kiraia (AZAKI) Lindi zina matumaini kuhusu manufaa ya mradi wa LNG. Wanaona LNG kama nishati mpito inayoweza kusaidia safari ya Tanzania kuelekea vyanzo vya nishati safi, ingawa wanakubali changamoto za kimazingira zinazotokana na miradi ya gesi asilia. AZAKI zinatetea mabadiliko ya taratibu za nishati kuelekea uchumi usio na kaboni, na pia zinafikiria kuwa kuna uwezekano wa kuunda hali ya kutegemeana kiviwanda kati ya sekta ya gesi asilia na sekta ya kilimo, ambayo inaweza kunufaisha wanajamii waliopo.

Sauti za wanajamii na muktadha wa kisiasa na kimaamuzi unaonesha hali ngumu ya utekelezaji wa mradi. Ingawa kuna matarajio makubwa ya fursa za kiuchumi zitakazotokana na mradi, pia kuna wasiwasi mkubwa kuhusu utekelezaji wake kutokana na ucheleweshaji. Hivyo, kadiri siku zinavyoenda, ni muhimu kwa serikali kushughulikia hisia hizi za wanajamii ili kuimarisha uhusiano na kukuza uaminifu kwa maendeleo ya muda mrefu ya mradi.




***Wanajamii wa Lindi katika warsha iliyoandaliwa na HakiRasilimali***

## Muundo wa Nishati Mpito Unaozingatia Haki

Asasi za Kiraia kama vile HakiRasilimali (HR) zimekuwa zikishirikiana kikamilifu na Wabunge nchini Tanzania ili kuleta na kuongeza hali ya uwajibikaji na usimamizi ndani ya sekta ya mafuta na gesi. Katika kuchochea na kuendeleza uwajibikaji na usimamizi, wabunge walihusishwa katika uwasilishaji matokeo ya utafiti uliofanywa na HakiRasilimali. Utafiti huo ulikuwa na lengo la kuangazia athari za mradi wa gesi asilia katika mazingira, pamoja na athari za kijamii na kiuchumi, kulingana na kasi ya mabadiliko ya kidunia kuelekea matumizi ya nishati safi, kwa lengo la kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi. Mchoro unaofuata unaonesha mambo muhimu ya kuzingatia katika utelekelezaji wa miradi ya nishati mpito kwa ajili ya kuongeza na kuendeleza uwajibikaji na usimamizi wa haki katika utekelezaji wa mradi wa gesi asilia nchini Tanzania. Mambi hayo ni:

Haki ya utambuzi inamaanisha kuwa jamii zinazoguswa na mradi moja kwa moja zinastahili kutambuliwa kimataifa ili kuongeza ushiriki wao katika miradi inayoendelea. Ingawa wawekezaji na Serikali ya Tanzania wamefanikisha mchakato mzima wa fidia kwa wale walioguswa na mradi wa gesi asilia, ni muhimu kuwa na sera, kanuni, na miongozo inayowagusa wanajamii wa eneo la mradi ili kulinda manufaa yao. Kipaumbele cha kwanza lazima kiwekwe kwa wanajamii wanaotoka eneo la mradi husika, badala ya dhana ya kwamba kila raia atafaidika na mradi. Aidha, manufaa ya uwekezaji hayapaswi kwa kiasi kikubwa kumnufaisha mtu ambaye haguswi moja kwa moja na mradi. Ni vyema faida na manufaa zianzie kwa jamii husika. Kutokufanya hivyo ni sawa na kutoitambua jamii inayotoka katika maeneo ya utekelezaji wa mradi.

Haki ya Uimarishaji inasisitiza ulazima kwa wawekezaji na Serikali ya Tanzania (GoT) kuhakikisha kuwa jamii inatendewa kwa heshima inayostahili, ikiwa ni pamoja na kuirejesha jamii katika hadhi yake ya awali kabla ya mradi. Jitihada za kuwezesha maendeleo endelevu katika jamii inayohusishwa na mradi zinapaswa kuelekezwa katika kujenga uwezo wa ndani kwa wanajamii, kuongeza ufahamu na elimu, na kuchagiza muingiliano wa viwanda vya ndani.

Haki ya Ugawaji inasisitiza umuhimu wa uzingatiaji haki katika mgawanyo wa faida zinazopatikana kutoka kwa mradi, ikichukulia madhara na manufaa ya mradi wa gesi asilia. Kama taifa, ni muhimu kukamilisha mazungumzo ya makubaliano kuhusu utekelezaji wa mradi wa gesi asilia na kuhakikisha kuwa manufaa ya mradi yanagawanywa kwa usawa na haki.

Haki ya Utaratibu inahusisha mikataba inayoingiwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Inahusiana kwa karibu na bei ya mafuta, ambayo hubadilika kimataifa na inaweza kusababisha changamoto za kimasoko. Hivyo, suala la kutokuwa na utulivu wa bei ni lazima lizingatiwe wakati wa kuingia mikataba ya muda mfupi na mrefu katika mradi, hasa kwa kuzingatia soko linalopatikana katika Bara la Asia ya Mashariki.

Mikataba ya muda mrefu inapaswa pia kujumuisha vifungu vya ukaguzi wa bei ili kutoa ulinzi dhidi ya mabadiliko makubwa ya hali ya soko. Kuna uhitaji wa kuwepo kwa mpangilio wa bei mseto unaohusisha sehemu ya bei ya mafuta na bei ya gesi. Kwa maana nyingine, ni muhimu kuwa na kipimo halisi cha bei ya gesi ili kusaidia taifa kuepukana na changamoto za bei za masoko na kuendelea kunufaika kiuchumi.




*Kielelezo cha 1: Nguzo za Nishati Mpito Wenye Haki*

Kwa ujumla, ingawa mradi wa gesi asilia (LNG) nchini Tanzania una manufaa makubwa ya kiuchumi, utekelezaji wake umeambatana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi ni pamoja na changamoto za kisiasa na kimaamuzi, matarajio yasiyo kuwa na uhalisia kutoka kwa jamii, na changamoto za kimazingira.

Uchechemuzi wa hali ya juu na utawala bora ni mambo mawili muhimu katika kukabiliana na changamoto hizi. Hii itahakikisha uwazi, usawa katika mgawanyo wa manufaa, na maendeleo endelevu ya jamii inayohusika na mradi. Kwa kushughulikia masuala haya kupitia muundo wa nishati mpito uliowasilishwa, Tanzania inaweza kusimamia mradi wa gesi asilia kwa ufanisi na kupelekea ukuaji wa muda mrefu wa kijamii na kiuchumi, huku ikipunguza athari mbaya za kijamii na kimazingira.



1. Marekani yaionya Tanzania Kuhusu Kuchelewa kwa Mradi wa Gesi Asilia (LNG) ( The Citizen)
2. Mustakabali wa LNG nchini Tanzania: Je ni Mtazamo Mzuri? (The Citizen)
3. Tanzania inatafuta washauri kwa ajili ya mradi wa gesi ailia wa dola milioni 30 (The East African)
4. Equinor, Shell na Exxon Wakubaliana Kuhusu Mradi wa LNG na Tanzania (Reuters)
5. Ukosefu wa usimamizi madhubuti unahatarisha uwezekano wa mradi wa LNG wa Tanzania (The Chanzo)
6. Sababu ya kukamilika kwa mradi wa LNG kuchukua muda mrefu zaidi (The Citizen)
7. Ucheleweshaji wa Mradi wa LNG Tanzania kutokana na Serikali kutaka kubadili masharti (Oedigital.com)
8. Wataalamu Watoa Wito wa Tahadhari Tanzania Inapoandaa Sheria Maalum kwa ajili ya Mradi wa LNG (The Chanzo)
9. Wadau Wanahoji Ukimya wa Utekelezaji wa Mradi wa Gesi Asilia (LNG), wakiitaka serikali Kuharakisha Mchakato Huo (The Chanzo)
10. Jamii wakazi Watafuta Elimu Kuhusu Mradi wa LNG Wenye Thamani ya Mabilioni ya Dola (The Citizen)
11. Serikali yatia saini Mkataba wa Awali wa Mkataba wa Serikali Mwenyeji (HGA) kwa ajili ya mradi wa LNG (PURA)




HakiRasilimali
Enhancing Transparency & Accountability of the Extractive Industry in Tanzania
IPIS
BHRT
BUSINESS AND HUMAN RIGHTS TANZANIA
Avocats Sans Frontières
ASF